MUKUSANYO WA WASULTANI WAMBOTE
WA SECTEUR BABILA-TETURI
TERRITOIRE DE MAMBASA
C/o

Etabe 3°, 28/02/98

PROJET PYGMEES - ETABE
DIOCESE BUTEMBO - BENI
NORD KIVU
REPUBLIQUE DEM. CONGO

Kwa Wabwana Waziri pa **Kinshasa**

+ Bw Waziri
  Min. de l'Environnement
+ Bw Waziri
  Min. des Affaires Sociales
+ Bw Waziri
  Min. des Affaires Coutumieres

JAMBO: Maulizo na mashtaki
ya Wambote wa Territoire
ya M A M B A S A .

Waheshimiwa Wabwana Waziri

Sisi, Wasultani wa Wambote, ambao signatures ziko huku chini, tunawatumia mashtaki yetu ya kushirikiana na wabwana wamoja, kama Mbazasi mmoja wa **BUTEMBO**, Bwana Administrateur titulaire wa MAMBASA, Sultani wa Collectivité ya BABOMBI, Sultani wa Secteur ya BABILA-TETURI, na wenginevyo, ambao tunawashtaki kwa matendo yao ya kutukosea haki yetu ya asili ya Congolais.

Mwanzoni mwa mwezi wa Febuari wamefika huku Teturi wabwana wawili wa jimbo la Thailandya, kwa kutazamia moele miitu ili wapate kujenga "usine" yakukata na kupasua mbao za miti ya bei ya miitu yetu.

Ndio sababu wameisha kuunda "comité" yao, ambao inakamata pia wabwana wale tuliowataja hapa juu.

Katila mambo yale yote, mtu hata mmoja aliwaza kutuuliza sisi Wambote, warithi wa kweli na wa haki ya asili ya miitu hii yote, na mtu hata mmoja aliwaza hatari mahututi maka kifo chetu sisi wote Wambote itakayotutokea kwa projet ile, kwani mwitu ni msinji wa maisha yetu!

**Sisi** hatukatae maendeleo na usitawi: kuitikia kwetu Projet Pygmées-Etabe ndi**a** alama wazi! Sisi tunalaumu mpango wowote juu ya mwitu wetu, mpango ambao akuna faida kwetu isio ile ya kuwa watumwa wa kazi ya chinichini.

Mwishoni tungalipenda kujua kama "projet" ile tunaolaumu inajulikana kweli kwa Wakubwa wa Serkali kule Kinshasa.

Na kitumaini cha kupata habari ya kama Wakubwa wa Serkali wapigania kulinda sheria ya haki yetu na watukinga katika hatari ya kupotea lote sisi pamoja na asili yetu, tunawasihi, Waheshimiwa Waziri, mupokee masalimio yetu na matakio yetu ya kazi njema.

SISI WASULTANI WAMBOTE WA SECTEUR BABILA-TETURI (TERR. MAMBASA)

| | |
|---|---|
| MESELE Sultani wa ETABE 1° | s/ |
| LAUSU Sultani wa KALUNGWE | s/ J.P. BARUTI (Chef Adjoint) |
| APYOMBE Sultani wa ETABE 2° | s/ Abeli: ABELI (Chef Adjoint) |
| SINGA Sultani wa KADODO | s/ |
| J.P.BESEY Sultani wa MAFEMBU | s/ |
| SAMUNYONGE Sultani wa MAMAHA | s/ |
| MIFO Sultani wa MAYODI | s/ Absent |
| ABELI Sultani wa MAULO | s/ |
| MBEMBE Sultani wa TESEMA | s/ NDJOBINE (Chef Adjoint) |
| ELUBU Sultani wa MAMBE | s/ KITAMBALA (Chef Adjoint) |
| SALAMBONGO Sultani wa MAKODU | s/ |
| SOMA Sultani wa SANGENGELU | s/ |
| SOKO Sultani wa KLEKE | s/ ALOMBI (Chef Adjoint) |
| MBOLU Sultani wa MASURU | s/ |
| LYOMBO Sultani wa MAPOYO/MIIUNGA | s/ ABSENT |
| TEKEYO Sultani wa MAMANGBA | s/ KIBELENGE (Chef Adjoint) |
| PABUMBE Sultani wa MENGANGO | s/ |
| MAIFGO Sultani wa PELUPELU | s/ AYALI (Chef Adjoint) |
| MUKONDJI Sultani wa ASYEFU | s/ |
| MUSAPAA Sultani wa MASONGO | s/ |
| MBILIBILI Sultani wa MAMAZI | s/ |